

MNADA WA HADHARA

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 mnamo Septemba 2012, ikiwa na lengo la kutoa huduma za kifedha kuititia kongani na minyororo ya thamani kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kimkakati katika kilimo.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inawatangazia Wananchi wote kuwa, Benki itauza kwa njia ya mnada wa hadhara vifaa chakavu ikiwemo magari, samani za ofisi, vifaa vya TEHAMA na vifaa vingine katika ofisi za Benki makao makuu, Dar es Salaam.

MALI ZINAZOUZWA

- Magari
 - Toyota Land Cruiser (1)
 - Ford Ranger (2)
- Samani za Ofisi
- Vifaa vya TEHAMA
- Vifaa Vingine

TAREHE YA MNADA

Ijumaa, 09 Februari
2024

MAHALI

TADB Makao Makuu (HQ),
Kiwanja Na. 84, Barabara ya
Kinondoni,
S. L. P. 75835, DSM.

MASHARTI YA MNADA

- Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
- Malipo ya vifaa chakavu ni asilimia mia moja (100%) na mteja atatakiwa kuondosha vifaa chakavu aliyonunua siku ya mnada.
- Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana “deposit” isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya bei na atatakiwa kukamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuza na amana iliyolipwa haitarudishwa.
- Mnunuzi wa gari, atatakiwa kuondoa au kuchukua mali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
- Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada husika kuanzia saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00).
- Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00) katika ofisi za Benki Makao Makuu kama iliyotajwa hapo juu.

Imetolewa Na,

Mkugurugenzi Mwendeshaji,
Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania
(TADB)

